**HOTUBA YA KATIBU MKUU WA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, SUSAN MLAWI YA KUMKARIBISHA MGENI RASMI KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA 14 CHA MAAFISA MAWASILIANO SERIKALINI KATIKA UKUMBI WA AICC, ARUSHA MACHI 12, 2018.**

**Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;**

**Mhe. Fabian Gabriel Daqarro, Mkuu wa Wilaya ya Arusha na Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa;**

**Dkt. Hassan Abbasi, Mkurugenzi, Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali;**

**Ndugu Paschal Shelutete, Mwenyekiti wa Chama cha Maafisa Habari Serikalini (TAGCO);**

**Ndugu Alvaro Rodriguez, Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa Tanzania,**

**Ndugu Elishilia Kaaya, Mkurugenzi Mwendeshaji wa AICC ambaye pia ni Mwenyeji wetu;**

**Viongozi wa Serikali mliojumuika nasi hapa;**

**Watendaji Waandamizi wa Serikali mliopo hapa;**

**Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano Serikalini,**

**Waandishi wa Habari,**

**Mabibi na Mabwana,**

**Habari za Asubuhi**

*Mheshimiwa Mgeni Rasmi;*

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama na kutuwezesha kufika hapa Arusha salama kwa ajili ya Mkutano huu wa kimkakati wa Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano Serikalini. Naamini kuwa sote tupo tayari kiakili na kiafya kufanikisha shughuli za wiki hii.

Pili napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuja kufungua rasmi mkutano huu. Tunakushukuru sana.

*Mheshimiwa Mgeni Rasmi;*

Mkutano huu ambao punde nitakuomba utufungulie rasmi, umewaleta pamoja Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano takribani 300 kutoka Wizara, Taasisi za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao watabadilishana uzoefu, kujifunza na kujadili Mada mbalimbali zitakazowajengea uwezo na weledi katika kuisemea na kuitetea Serikali hasa katika kipindi hiki ambacho Wananchi wana hamasa kubwa ya kutaka kufahamu mambo mbalimbali ambayo Serikali inayatekeleza. Mkutano huu ni wa 14

toka tulipoanza utaratibu wa kukutana kila mwaka toka mwaka 2005. Kauli mbiu ya Mkutano huu ni **"Mawasiliano ya Kimkakati yanachagiza vipi uchumi wa Viwanda?"**

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi,***

Mkutano wa mwaka huu ni tofauti na mikutano iliyofanyika miaka ya nyuma kwa sababu washiriki watapata fursa ya kufanya majadiliano zaidi tofauti na utaratibu uliozoeleka wa kusikiliza Mada tu bila kuwa sehemu ya majadiliano ya Mada husika. Pamoja na maboresho hayo, katika Mkutano wa mwaka huu, kutakuwa na Mada mbalimbali zitakazo jadiliwa. Baadhi ya Mada hizo ni: *Umuhimu wa Mawasiliano ya Kimkakati katika Kuisemea Serikali na Tathmini ya Utendaji katika Mwaka 2017*; *Maadili na Usalama katika Kazi ya Kuitangaza na Kuisemea Serikali; Wajibu wa Maafisa Habari katika Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Maafa; Misingi na Utaratibu katika Upigaji Picha za Habari; Matumizi Sahihi ya Lugha Adhimu ya Kiswahili katika Uandishi wa Taarifa za Serikali; pamoja na Uzoefu na Mbinu za Kupambana na Dharura katika Kuisemea Serikali*. Aidha, Washiriki watapitishwa na kuelezwa wajibu wao kwa mujibu wa Sheria mpya

zilizotungwa hivi karibuni: *Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016* na *Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa Na. 6 ya mwaka 2016.*

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Idara ya Habari Maelezo chini ya uongozi wa Dkt. Hassan Abbasi na TAGCO chini ya uenyekiti wa Bw. Pascal Shelutete kwa uratibu na kufanikisha mkutano huu. Hongereni na asanteni sana.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Nipende  kukufahamisha kuwa mkutano wa mwaka huu umekuwa na hamasa kubwa si tu kwa Maafisa Habari wenyewe, bali hata kwa viongozi wa Serikali, Mashirika ya Kimataifa na Sekta Binafsi na wengi kuomba kushiriki nasi. Ndio maana katika utambulisho umesikia uwepo wa viongozi mbalimbali kuanzia Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na Taasisi za Umma, Taasisi za Kimataifa na Sekta Binafsi.

Hamasa hii imejitokeza pia katika uwasilishaji wa Mada na tulipata changamoto kuamua Mada zipi zitolewe katika Mkutano na zipi zitafutiwe nafasi katika Mikutano ijayo. Miongoni mwa watoa Mada

atakuwepo Prof. Elisante Ole Gabriel, Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara. Pia wapo Watendaji Wakuu wa Taasisi mbalimbali za Umma, Kimataifa watakaowasilisha Mada mbalimbali akiwemo Alvaro Rodriquez, Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN) na timu yake.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi,***

Wadhamini wengi wameonyesha ushirikiano mkubwa na wamejitoa kufanikisha Mkutano huu. Kama unavyoona mabango yao yamependezesha ukumbi Ukumbi huu. Aidha, vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii vimeshiriki kusaidia kuutangaza Mkutano huu. Tunawapongeza na kuwashukuru sana wote waliojitokeza kushirikiana nasi kwa namna mbalimbali.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Washiriki ni mabalozi wa kuitangaza nchi yetu. Hivyo, katika Wiki hii pamoja na mambo mengi ya kujifunza wakiwa katika Ukumbi huu pia watafanya mambo mawili muhimu. Kwanza, watatembelea Shule ya Msingi Laiboni iliyoanzishwa na Mzee wa Laiboni kwa ajili

ya familia yake na sasa inasaidia jamii kubwa inayomzunguka.Katika ziara hiyo watatoa misaada mbalimbali. Pili, ili kukuza utalii wa ndani, watatembelea Hifadhi ya Taifa ya Tarangire ili kujionea vivutio tulivyo navyo.

Nipende kusisitiza, sisi kama Wizara inayosimamia Habari hatuna budi kuwa mstari wa mbele kuisemea Serikali kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati hasa katika kipindi hiki ambacho kimekuwa na upotoshwaji wa taarifa za utendaji wa Serikali. Tutaendelea kusimamia weledi, Sheria, Kanuni na Taratibu katika kusimamia Sekta hii muhimu.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi,***

Baada ya kusema haya, kwa heshimi na taadhima naomba sasa nikukaribishe ili utoe Hotuba yako, kutufungulia rasmi Kikao Kazi hiki cha 14 cha Maafisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano Serikalini, kutoa vyeti kwa Wadhamini wa Mkutano huu na kuzindua tovuti ya TAGGO ambayo itakuwa ni nyenzo muhimu ya kurahisisha mawasiliano na upatikanaji wa taarifa zinazohusu masuala

mbalimbali ya maafisa Habari, Mawasiliano, na Uhusiano Serikalini. Ufunguzi huu, kama tulivyojulishwa kwa sasa unatazamwa sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi kupitia *MAELEZOTV* iliyoko mtandaoni.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi karibu sana.